**Mpango wa Kimataifa wa Mwanafunzi wa Druid Hills Waweka Vimiminio vya Mafuta ya Kuzuia Miali ya Jua kwenye Maeneo ya Umma katika Kaunti ya DeKalb**




Vijana wadogo wa shule ya kati wanaweza kuwa na mafadhaiko mengi kutokana na changamoto za kubalehe na mabadiliko mengine katika miili yao. Mojawapo ya wasiwasi wa kawaida ni kuonekana kwa chunusi, ambazo mara nyingi hufanya wenzao wawakejeli. Inaweza kuwa changamoto kwa vijana wadogo kuelewa kile kinachoendelea kwenye ngozi yao na jinsi ya kukabiliana na changamoto hii.

Wakati wa shule ya kati, Ellis Schroeder alikabiliwa na tatizo mbaya zaidi la ngozi lilaloitwa rosasia(uwekundu wa muda mrefu), ambalo bado analo. Rosasia ni ugonjwa wa kawaida wa ngozi unaoathiri takriban Wamarekani milioni 16, kulingana na Muungano wa Madaktari wa Ngozi wa Marekani (AAD). Na hivi sasa, akiwa mwanafunzi wa gredi ya 11 katika Druid Hills High School, Ellis mara nyingi hupata ngozi nyekundu na upele kwenye pua na mashavu kutokana na tatizo hili la ngozi la muda mrefu.

“Kuna visa vingi vya kutojiamini katika shule ya kati. Nimewahi kuitwa kutoka foleni na mwalimu wangu mmoja katika darasa la sayansi, na mwalimu akaniuliza nilikuwa na tatizo gani usoni,” Ellis alisema. “Wenzangu darasani walikuwa tayari wakiniuliza kama nilikuwa nimejipaka mafuta ya kuweka uwekundu au nilikuwa nimejipodoa na kuniuliza nina matatizo gani usoni. Hilo liliathiri sana kiwango changu cha kujiamini.”

Ellis alianza kuchunguza tatizo lake na matatizo mengine ya ngozi ambayo huwaathiri vijana wadogo. Alikagua tafiti kutoka kwa madaktari wa ngozi na kutazama video kwenye YouTube kuhusu rosasia na matatizo mengine kama hayo ya ngozi. Alijaribu kuwaeleza wanafunzi

wenzake kuhusu hali yake lakini akagundua kuwa hawakuelewa umuhimu wa afya nzuri ya ngozi.

“Hatupati elimu ya kina sana ya afya, haswa kuhusu ngozi yetu,” Ellis alisema. “Hilo lilinifanya nianzishe shirika linaloitwa DermaTeens, ambalo limejitolea kuwaelimisha vijana kuhusu afya ya ngozi na kuhimiza usalama wa miali ya jua.”



Shirika la DermaTeens lilianzishwa mnamo mwaka wa 2021 kama mradi wa kutunga makala za habari kuhusu matatizo anuwai ya ngozi. Ellis alitafiti taarifa kutoka kwa Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa na AAD ili kutunga makala za kuelimisha. Kulingana na muungano wa Pediatric Partners of Augusta, baadhi ya matatizo ya kawaida ya ngozi ambayo huathiri vijana ni pamoja na chunusi, ukurutu, uvimbe, psoriasisi, na rosasia.

Ellis alipanua shirika la DermaTeens hadi vijana 50 duniani kote baada ya kushuhudia ongezeko la usomaji wa makala. Mfumo huu unanuia kushiriki habari kuhusu afya ya ngozi na hushughulikia ukosefu wa usawa wa kiafya unaoathiri vijana.

“Hiyo inatuhamasisha kuanzisha mipango tofauti,” Ellis alisema. “Tuliunda vifurushi vya ulinzi wa miali ya jua, kifurushi cha bidhaa za usafi, na vitu muhimu kwa Makao ya Wasio na Makazi ya Atlanta Mission.”

Shirika la DermaTeens kwa sasa linahusika katika miradi kadhaa, ikiwa ni pamoja na kuweka vimiminio vya mafuta ya kuzuia miali ya jua kwenye maeneo ya umma. Mnamo mwaka wa 2022, Ellis aliungana na shirika la IMPACT Melanoma kufadhili na kuweka vimiminio kumi na

viwili vya mafuta ya kuzuia miali ya jua katika maeneo ya umma kwenye Bustani ya Zonolite katika eneo la Druid Hills. IMPACT Melanoma ni shirika kuu lisilo la faida nchini Marekani linalojitolea kupunguza kwa kiasi kikubwa matukio ya saratani ya melanoma na kuokoa maisha.

IMPACT Melanoma hutoa vimiminio vinavyobebeka na visivyo vya kugusa vya mafuta ya kuzuia miali ya jua katika mpango wake wa "Our Safe Skin at Work"(Ngozi Zetu Salama Kazini). Akiwa na shauku kama kawaida, Ellis aliandaa tukio la uchangishaji ili kuchangisha pesa kwa ajili vimiminio hivi vya mafuta ya kuzuia miali ya jua na kuweza kuviweka kwenye Bustani ya Zonolite katika msimu uliopita wa kiangazi.

"Niliwasiliana na shirika la [IMPACT Melanoma] na kuwaambia nilitaka kutekeleza mpango huu kwenye jamii yangu," alisema. "Ni mradi ninaoendesha mwenyewe ambapo lazima niombe ufadhili na ushirikiano na idara za bustani na burudani."

Ellis aliwasiliana na makamishna wa Kaunti ya DeKalb kupitia barua pepe kuhusu mradi wake. Kamishna Ted Terry alijibu mara moja na kumjumuisha Chuck Ellis, mkurugenzi wa Idara ya Bustani na Burudani ya Kaunti ya DeKalb kwenye mazungumzo hayo. Sasa wanashirikiana kuweka vimiminio vya mafuta ya kuzuia miali ya jua katika eneo la Toco Hills, ambako Ellis anaishi, kwa ushirikiano na Tume ya Vijana ya Kaunti ya DeKalb – shirika ambalo Ellis ni sehemu yake. Uwekaji wa vimiminio hivi umepangwa kufanyika baadaye msimu huu wa machipuko. Kisha, wanachunguza uwezekano wa kuweka vimiminio vya mafuta ya kuzuia miali ya jua kwenye vituo vya gofu na tenisi katika kaunti nzima na kando ya vijia.

Shirika la DermaTeens lina dhamira ya kupambana na ueneaji wa habari potofu kuhusu afya ya ngozi. Kwa mfano, kuna dhana potofu ya kawaida kwamba Waafrika Wamarekani hawahitaji kujipaka mafuta ya kuzuia miali ya jua. Hata hivyo, hii si kweli. Kulingana na AAD, watu wa rangi zote, ikiwa ni pamoja na wale walio na ngozi ya kahawia na nyeusi, wanaweza kupata saratani ya ngozi. Kwa hiyo, watu wa rangi wanapaswa kujipaka mafuta ya kuzuia miali ya jua ili kupunguza hatari ya saratani ya ngozi.

"Visa vya mamangu kugunduliwa kuwa na saratani iliyoenea ya matiti na kisha shangazi yangu kugunduliwa kuwa na saratani ya melanoma vilinifanya nione uzito wa afya ya ngozi na jinsi ni muhimu kwa watu wa rika na rangi zote kuwa na mbinu salama za kujikinga na miali ya jua na kuzingatia kuhakikisha kuwa afya ya mwili wote ni bora ili kuzuia matatizo kama haya," alisema Ellis.

Ellis alisema anahisi kuwezeshwa anapowafundisha wenzake na wengine kuhusu afya ya ngozi, na hivyo kumtia moyo kuzingatia kusomea utaalamu wa afya ya umma. Anatumai kuwa kazi yake pia itawahimiza vijana wengine kuleta mabadiliko chanya katika jamii yao, haswa kuhusiana na maswala wanayopenda sana.

“Ukichunguza kwa kina mambo yanayoendelea karibu nawe, unaweza kugundua maswala yanayokuvutia ambayo yanakukera au kukasirisha na utafute njia za kuyarekebisha,” alisema Ellis. “Inaweza kuhisi vizuri sana.”

Kwa habari zaidi kuhusu shirika la DermTeens, tafadhali bofya viungo vilivyo hapa chini.

- https://dermateens.wixsite.com/dermateens
- https://www.instagram.com/dermateens/
- https://www.youtube.com/watch?v=nxqgtIJ_B3A
- https://www.linkedin.com/company/dermateens
- https://impactmelanoma.org/meet-ellis-schroeder-your-skin-is-in-ambassador-and-founder-of-dermateens/